



## AL-HUDAA [UONGOFU]

25/= Ksh

Volume 26, Issue 3

8th Safar 1434

21st Dec, 2012



## UTAPATA VIPI USHINDI KATIKA MAISHA YAKO KWA MUONGOZO WA KITAAB NA SUNNAH

NA: SHEIKH MUHAMMAD SAALIH AL-MUNAJJID

## WASILIANA NASI

SIMU (+254) 721473181

Mombasa, Kenya

E-MAIL Info@qssea.net

Web Site: <http://www.qssea.net>

## YALIYOMO KATIKA JARIDA LA WIKI HII

KUTAFUTA SA'AADA 1 - 4

## HABARI ZA MAZINGIRA YA WAISLAMU KWA MUKHTASAR

**Kuna uwezekano kwamba serikali ya Syria inaweza kushindwa na majeshi ya upinzani wakati wowote ule, naibu waziri wa masuala ya kigeni wa Urusi amesema.** Wanajeshi wa rais Bashar al-Assad "wanazidi kupoteza maeneo zaidi kila wa leo", Mikhail Bogdanov alisema Alhamisi, kulingana na mashirika ya habari ya Urusi.

Urusi imekuwa mmojawapo wa washirika wakuu wa serikali ya Bwana Assad.

Wakati huohuo, Urusi inafanya mipango ya kujitayarisha kuwahamisha maelfu ya Warusi toka Syria, Bwana Bogdanov alisema.

**Mlipuko**

"Kwa kweli hatuwezi kutupilia mbali uwezekano wa kwamba waasi wa Syria wanaweza kushinda," Bwana Bogdanov alisema.

Nchini Syria kwenyewe, vyombo vya habari vya serikali vimeripoti kutokea kwa mlipuko katika eneo la Qatana, jijini Damascus, ambalo limewaua watu 16, wakiwemo watoto saba.

**[BBC London]**

**SUALA :** Vipi waweza kufaulu na kupata mafanikio katika ulimwengu huu na Akhera? Ni kufaulu kupi na ufanisi upi ambao Uislamu wataka Ummah wa Kiislamu upate katika Ulimwengu huu

**JAWABU :** Alhamdulillah: kutulia kwa akili, kutoshelezeka, furaha na uhuru kutokana na wasiawasi na hamu...haya ndio anayo yataka kila mtu, na hizi ndio njia ambazo watu wanaweza kuwa na maisha mazuri na wakapata furaha kamili na kuterema. Ziko njia za kideeni za kuyapata hayo, na za fitra na zakutedewa kazi, lakini hakuna awezao kuyajumuisha yote hayo ila Muumin; ingawaje watu wengine waweza kuyapata baadhi,

watayakosa mengine.

Hapa twafuatisha mukhtasari wa namna yakulipata lengo hili ambalo kila mtu alifanyia juhudi. Katika hali nyingine, wale watakao yakosa yote watakuwa na maisha ya huzuni na uzito. Nakuna wengine wako katikati, kulingana na anavyo weza kuzpata namna. Hizi ni miongoni mwa namna hizo:

**1-IMAAAN NA MATENDO MEMA:** hii ndio namna ilio kubwa na yamsingi zaidi. Allaah Asema: **[Mwenye kutenda mema ,mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumin**

*(Endelea kwenye Uk. 2)***SEMINA YA UKUMBUSHO WA SHEIKH AL-AMIN BIN ALI AL-MAZRU'I**

"THE QUR'AN & SUNNAH SOCIETY OF EAST AFRICA" WANAWAALIKA MIHADHARA YA KI-'ILMU KATIKA MASJID MAZRU'I KUANZIA TAREHE 24<sup>th</sup> DEC – 27<sup>th</sup> DEC, 2012

[SIKU NNE]

**MAUDHUI NA WAHADHIRI:**

1. TAWHEED - ABU AHMAD
2. NDOTO KATIKA UISLAMU - USTADH ISMAA'IL
3. SABABU ZA UTESI MAJUMBANI - SHEIKH HAMMAD KASSIM
4. HESHIMA YA MWANAMKE - USTADH SHARIFF

**WAKATI WA MIHADHARA**

KUANZIA BA'DAL ASR MPAKA ISHAA'

**WANAUME WATAKUWA NDANI YA UKUMBI WA MSIKITI NA WANAWAKE WATAKUWA JUU [WANAPOSWALI].**

(Endelea Kutoka Uk. 1)

**Tutamhuisha maisha mema; tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda @An-Nakhl 16:97]**

Allaah Atueleza sisi na Kutuahidi sisi kuwa yoyote atakae jumuisha Imaan na matendo mema atakuwa na maisha mazuri na malipo bora katika ulimwengu huu na kesho Akhera. Sababu ya hilo liko wazi: wale wanao muamini Allaah-kwa imaan ya kikweli inao washajiisha kufanya matendo mema yanayo badili mioyo na tabia na kuwaongoza wao katika njia ilio nyooka katika maisha haya ya dunia na Akhera-wanafuata mienendo na mipango kwa namna ambayo wanapambana na kila kitu kitacho tokea kwao, ikiwa nisababu za furaha na kufurahika, au sababu za wasiwasi, hamu na msiba. Wanapambana na mambo hayo ambayo wapenda kuyakubali na kutoa shukurani kwayo, na kuyatumia kwa njia nzuri. Ikiwa watapambana nayo katika namna hii, ambayo yaunda ndani yao hali ya kishajiishwa kwa furaha na tamaa ya kuwa itaendelea na kuwa watalipwa kwa kushuru kwao, ambayo nimuhimu kwao kuliko mambo mazuri yanayo wapata. Na wanapambana na mambo mabaya, udhia na huzuni, kwa kujizuia na yale wanayo weza kujizuia nayo, kuyapoza wanayo weza kuyapoza, nakuyabeba kwa wema wa subira yale wanayoweza kuyaepuka. Hivyo kwa matokeo ya mambo mabaya wanapata faida kubwa, ujuzi, nguvu, subira na matarajio ya malipo bora, ambayo ndio muhimu na ambayo yaondosha mazito waliopitia na kuyabadilisha kwa furaha na matarajio ya zawadi na malipo ya Allaah. Mtume صلى الله عليه وسلم aliyanyesha haya katika hadeethi saheeh alipo sema: “Ni hali iliyo nzuri gani ya muumini, kwani mambo yake yote ni mazuri. Likimtokea jambo zuri, atoa shukurani kwalo na hilo ni zuri kwao; likimtokea jambo baya, alibeba kwa subira, na

hilo ni zuri kwake. Hili halimuhusu yoyote isipokuwa muumini.” (Muslim #2999). Mtume صلى الله عليه وسلم alitueleza kuwa muumini mara zote afaidika na malipo ya matendo yake yaongezeka ikiwa lolote litamtokea, zuri au baya.

**2-KUWA MWEMA**-Kuwa mwema kwa watu kwa maneno na vitendo, na kufanya mazuri katika mazuri yote. Hi nimoja katika namna ya kuondosha udhia, kuhangaika na wasiwasi. Kwa hili yamaanisha kuwa Allaah andosha udhia na kuhangaika kutoka kwa waumini na watu watabia ya hali ya juu. Lakini muumini analo fungu kubwa katika hayo, na atambulikana kuwa wema wake kwa watu yatokamana na ikhlasi yake na matarajio alionayo kupata malipo kwa Allaah, kwahivyo Allaah amfanyia rahisi kuwa mwema kwa wengine kwa sababu ya matarajio yake kuwa kutakuja kwa ajili ya hayo mazuri na kuyafukuza mabaya, kwa njia ya ikhlasi yake na matarajio yake yakulipwa na Allaah. **[Hakuna kheri katika mengi ya wanao shauriyana kwa siri, isipo kuwa kwa yule anaye amrisha kutoa sadaka, au kutenda mema, au kupatanisha baina ya watu. Na mwenye kufanya hayo kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu basi tutakuja mpa ujira mkubwa. @An-Nisaa 4:114]** Fungu moja miongoni mwa malipo hayo ni afueni kutokamana na mazito, kuhangaika, shida na dhiki nyingine.

**3-KUTAFUTA ILMU YENYE MANUFEEA** –namna nyingine yakufukuza wasiwasi inayotokamana na kutetemeka kwa baada ya kutishika na shida fulani na kuwa umeshughulishwa na mawazo ya usumbufu niku jishughulisha nafsi yako na matendo mazuri na kutafuta ilmu ya manufaa, kwani jambo hilo litazuia mtu kuduwa katika mambo yanayo sababisha wasiwasi. Kwa njia hii mtu aweza kusahau yenye kumsumbua, na yakumbabaisha, na aweza kuwa na furaha na akawa na nguvu. Hii ni namna nyingine ambayo waumini na wengine wanao kwa ujumla, lakini muumini atambulikana kwa imaan yake, ukweli na matarajio ujira wa Allaah anapo jishughulisha na ilmu hiyo ambayo

ajifunza au afunza, au na matendo mema ambayo atenda.

Kazi anayojishughulisha nayo yatakiwa iwe ni jambo alipendalo na kumstarehesha, kwa hilo laweza kwa uwezekano mkubwa kuleta matokeo yanayo tamaniwa. Na Allaah ajua zaidi.

**4-KUYAWAZA YALIO YA WAKATI**-jambo lingine ambalo lafukuza kubabaika na wasiwasi nikuyalenga mawazo yako yote juu ya siku iliyonawe, na usijali kuhusu siku za usoni na kuomboleza kuhusu yaliopita. Ndipo Mtume صلى الله عليه وسلم akajilinda kwa Allaah na kubabaika na majuto, majuto kwa mambo yaliopita ambayo mtu hawezi kuyafanya sawa wala kuyabadilisha, na kubabaika kunao weza kuja kwa ajili ya khofu ya siku za usoni. Kwahivyo mtu ayaweke mawazo yake juu yalio sasa, na kuzielekeza juhudi zako katika kuyaweka sawa yalio leo. Ikiwa mtu yuko juu ya hayo, hii ina maana kuwa atafanya mambo kisawasawa na kusahau kuhusu kubabaika na kujuta.

Wakati Mtume صلى الله عليه وسلم alikuwa akiomba du’aa au akiifundisha kwa Ummah wake, na vile vile kuwahimiza kuiomba nusra ya Allaah kwa neema Yake, alikuwa pia akiwahimiza kuyatafuta kwa juhudi yale mambo wanayo yaomba kwa juhudi yao na kusahau yale waliyo kuwa wakiyaomba yataondoshwa kutoka kwao. Kwa sababu du’aa nilazima zifuatane na matendo. Kwa hivyo mtu ni lazima afanye juhudi ya kupata kitakacho mfaa katika dunia na na dini yake. Na amuombe Mola wake kuzifanya juhudi zake zipate kuafikiwa, na atake msaada Wake katika hilo kama alivyo sema Mtume صلى الله عليه وسلم: “Fanya juhudi kwa lile litakalo kufaa na taka msaada wa Allaah, na usiwe bila ya uwezo. Lolote baya litakalo kutokea, usiseme, ‘lau kama ningelifanya kadhaa, basi jambo kadhaa lingetokea.’ Bali wafaa useme, ‘Qadara Allaah wa ma sha’a fa’ala (Allaah ameqadiria na alitakalo afanya kwa walimwengu) ‘ikiwa sivyo basi wafungua mlango kwa

(Endelea katika Ukurasa wa 3)



(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

shaytaan. [Muslim].

Mtume صلى الله عليه وسلم aliunganisha mambo ya juhudi ya kupata mazuri na mambo ya kutaka msaada wa Allaah na usijipe hisia za kuwa myonge ambazo zina madhara ya aina ya uvivu, na hali yakubali mambo yaliopita na ambayo yasha fanyika, nakuelewa kuwa qadari ya Allaah bila shaka itakuja kupita. Akaeleza kuwa mambo ni ya sampuli mbili:

**a-**Mambo ambayo mtu afanya juhudi yakuyapata au kuyapata yale awezao, au kuyafukuza au kuleta afueni kutokana nayo. Katika hali hiyo mtu nilazima afanye juhudi na vile vile atake msaada wa Allaah.

**b-**Mambo ambayo hayana uwezekano, kwahivyo ni lazima awe na kutuliza akili, ayakubali na ajitolee kwa qadari ya Allaah.. Bila shaka kuizingatia misingi hii kutaleta furaha na afueni kutokana na kubabaika na kuhangaika.

**5-DHIKR** –Miongoni mwa namna tukufu ya kutoshelezeka na kutulia na kuupata utulivu wa akili nikumkumbuka Allaah mno (**dhikr**) hilo lina athari kubwa ya kuleta kutoshelezeka na utulivu wa akili, na kuondosha kubeheneka na kuhangaika. Allaah Asema: [**Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!** @Ar-Raad 13:28]

Dhikr ina athari kubwa katika kulipata lengo hili kwa sababu ina athari haswa na kwa sababu ya tamaa inayo leta ya ujra (malipo)

#### **6- KUYAONDOSHA MAHANGAIKO**

–namna nyingine yakuleta furaha na kujipa nafuu ya kubabaika na kuhangaika nikufanya juhudi ya kuondosha mambo yanayo sababisha kubabaika na kupata mambo yaletayo furaha. Hilo laweza kufanywa kwa kusahau kuhusu mambo mabaya yalio pita ambayo hayawezi kubadilishwa, nakufahamu kupitisha

wakati juu yake nikupoteza wakati. Kwa hivyo mtu nilazima afanye juhudi ya kusimamisha yakuyafikiria hayo. Na vile vile ajisimamishe na kujihisi na fazaa za siku zijazo na kuwaza kuhusu umasikini, khofu na mabaya mengine anayo yafikiria kuwa atatokea kwake siku za usoni. Nilazima azingatie kuwa mambo yanayokuja ni kitu kisicho julikana, hawezi kujua ni zuri au baya litakalo tokea hayao yako mikononi mwa Allaah Aliye Hakimu mno, na yote wawezao kuyafanya waja Wake nikufanya juhudi yakuyapata mambo mazuri na kuyafukuza mabaya. Mtu nilazima azingatie akizigeuza fikra zake kutoka kwa kubabaika kuhusu siku zake zijazo na akamuamini Allaah kuingalia hali yake, nakuiweka akili yake mapumzishoni kuhusu hayo, akifanya hivyo, basi moyo wake utakauwa kaika salama na hali yake atakuwa bora na atapata afueni kutokamana na mahangaiko na wasiwasi.

Miongoni mwa namna zilizo na athari kubwa ya kupambana na kubabaika kuhusu siku zijazo nikuisoma du'aa hii ambayo Mtume صلى الله عليه وسلم alikuwa akiisoma: “Allaahuma aslih li deeni alladhi huwa ‘ismatu amri, wa aslih li dunyaaya allati fiha ma’aashi, wa aslih li aakhirati allati ilayha ma’aadi, waj’al al-hayaata ziyaadatan li fi kulli khayr, wa’l-mawta li min kulli sharr” (Ewe Allaah rekebisha majukumu ya deeni yangu ambayo ndio misingi ya maisha yangu, na rekebisha mambo yangu yadunia ambayo ndio maisha yangu, na nipe mazuri Akhera ambapo ndio maregeo yangu, yafanye maisha yangu yawe ni namna ya kukusnya mazuri, na uyafanye mauti ni afueni kwangu kutokamana na maovu) [Muslim #2720]

Na alikuwa akisema: “Allaahuma rahmataka arju fa la takilni ila nafsi tarfata ‘aynin wa aslih li sha’ni kullahu, laa ilaaha illa anta” (Ewe Allaah natumai rahma yako kwa hivyo usiniache mimi peke yangu, hata kwa mda mchache. Na yarekebishe mambo yangu yote. Hakuna kizuri ila Wewe) [Abu Dawood #5090 hasan al-Albani katika saheeh kalim al-Tayyib, p.49]

Ikiwa mtu atazitamka du’aa hizi, ziulizao kuwa mambo ya dunia na deeni yafanywe sawa na kurekebishwa, kwa kuwa na akili ilio makinika na ikhlaas ya nia, hali yakuwa wafanya juhudi yakuyapata hayo, Allaah atakupa uliyaomba, uliotumai, na uliojuhudika nayo, na atabadisha kuhangaika kwake kuwe ni raha na furaha.

#### **7-KUFIKIRIA KUWA LINGEKUWA**

**BAYA ZAIDI** –ikiwa mtu atahisi wasiwasi na kuhangaika, kwa sababu ya msiba, basi moja ya namna yakujiondoshea hayo nikufikiria hali ilio mbaya ambayo hayo yaweza kuelekea, na ajaribu kuyakubali. Atakapokuwa amefanya hivyo, basi najaribu kujitopoa kadri awezavyo. Kwa namna hii ya kukubali na bidii, atajiondoshea nafsi yake mahangaiko hayo na mababaiko, na badala yakubabaika atafanya juhudi ya kuleta mambo mazuri na kupambana na anayo yaweza katika mabaya.

Akikabiliwa na mambo yanayo sababisha khofu au uwezekano wa magonjwa au ufakiri, basi nayakabili hayo kwa kuwa na juhudi ya kuyakubali, au mazito kuliko hayo, kwa kutoshelezeka, kwa sababu akijiweka katika hali yakuikubali hali ambayo yaweza kuwa mbaya zaidi, ayapunguza matungu ya mambo na kuyafanya yaonekane kuwa si mabaya sana, haswa ikiwa atajishughulisha na mambo yakuyafukuza kadri yawewe wake. Na vile vile kujishughulisha kupata jambo zuri hilo litamsahulisha na kubabaika kuhusu janga lake, pia ataiboresha nguvu zake za kustahmili mambo mabaya, na aweke imani yake na mategemeo yake kwa Allaah. Bila shaka mambo haya yana faida kubwa katika kuleta furaha na utulivu wa akili, na vile vile kuleta matumaini ya ajra katika dunia hii na Akhera. Hili ni jambo linalo julikana sana kwa wengi wamekao lijaribu.

**8-KUVUMILIA MOYO**- kuvumilia kwa moyo na kuto sumbuliwa na mambo ya kudhania ambayo mawazo mabaya yaweza kuletwa kichwani. Wakati mtu ajiwachilia katika kuwaza kwake na akaiacha akili yake kusumbuliwa na mawazo, kama khofu, maradhi na mfano

(Endelea kutoka Ukurasa 3)

wake, au hasira na kurengwa iliyo chemka kwa mambo ya matungu, au kutarajia mambo mabaya na kupoteza mambo mazuri, hayo yatamjaza wasiwasi, kuhangaika, wazimu na maradhi ya mwili na kuanguka kimoyo, ambayo itakuwa na athari mbaya juu yake na inayo leta madhara mengi kama walivyo ona watu wengi. Lakini mtu akimtegemea Allaah na akamuamini Yeye, na hajiachii katika mawazo yake au kuyawacha mawazo mabaya yakamshinda, na akamtegemea Allaah na anatarajia neema yake, ambayo itafukuza mahangaiko yake na kubabaika, na yampa nafuu na afueni kubwa ya magonjwa ya akili na ya mwili. Yaampa nguvu za ajabu, utulivu na furaha kwa moyo. hospitali ngapi zimejaa wagonjwa wa akili wahasiriwa wa mawazo na fikra za madhara; mara ngapi mambo haya yamekuwa na athari katika mioyo ya watu wenye nguvu, licha walio madhaifu; mara ngapi yamewaelekeza katika ujinga na uwenda wazimu.

Yafaa ijulikane kuwa maisha yako yataandama gari la mawazo yako. Ikiwa mawazo yako ni yamambo yatakayo kuletea faida ya kilimwengu na dini katika mambo yako, basi maisha yako yatakuwa mazuri na yafuraha. Ama sivyo yatakuwa kinyume.

Mtu aliye salama kutokana na hayo yote ni yule aliye hifadhiwa na Allaah na kusaidiwa Naye kufanya juhudi ya kufanikiwa na yatakayo mfaidi na kumpa nguvu za moyo na kufukuza wasiwasi.

Allaah asema: **[Na humruzuku kwa jiha asiyo tazamia. Na anaye na anaye mtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenye Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake. @At-Talaq]**

Yaani, atatoshelezeka na yote anayo msumbua katika dini na ulimwengu wake. Atakaye mtegemea Allaah atakuwa na nguvu moyoni mwake na hata dhurika na chochote akiwazacho au kusumbuka na matokeo ya mambo, kwa sababu ajua haya ni matokeo ya udhaifu wa mwanaadamu na fitra aliyo umbiwa nayo

na khofu zisizo msingi. Pia ajua kuwa Allaah Amewahidi kutoshelezwa kwa wale wanao mtegemea Allaah kwa ukamilifu. Kwahivyo amuamini Allaah na anapata utulivu wa akili katika ahadi yake, na kwahivyo masumbuko yake na wasiwasi yaondoshwa; uzito wabadilishwa na kuwa wepesi, huzuni yabadilika kuwa raha, khofu yabadilika na kuwa salama. Twamuomba Allaah atuweke salama salimini, na atubariki kwa nguvu na uvumilivu wa moyo, nakumuamini Yeye kwa ukamilifu, kwani Allaah ameahidi mambo yote mazuri kwa wale watakao muamini na kumtegemea kwa ukamilifu, na amewahakikishia kuwa atawaondolea mambo yote mabaya na yenye madhara kutoka kwao.

Ikiwa mabaya yatakuwa au kuna khofu ya hayo, basi hesabi neema nyingi kutoka kwa Allaah ambazo bado wastarehe nazo, na hii itayafanya mambo mabaya yaonekana kuwa si mabaya sana. (tizama al-Wasaa'il al-Mufeeda li'l Hayaat al-Sa'eedah na Shaykh 'Abd al-Rahmaan ibn Sa'di) Ibn al-Qayyim aliyakusanya mambo kumi na tano ambayo kwao Allaah aondosha masumbufu na majuto. Nayo ni kama afuatavyo

Tawheed al-Ruboobiyyah (kuamini

Umoja wa Uungu wa Allaah)

Tawheed al-Uloohiyyah (Kuamini Umoja wa Uola wake)

Tawheed ya Ilmu na imaan (yaani

Tawheed al-Asma' wa'l\_Sifaat, kuamini kwa umoja wa majina na sifa)

Kumdhania Allaah kuwa yuko mbali na kuwadhulumu waja wake kwa sampuli yoyote, na kuwa hawezi kumuadhibu yeyote bila sababu juu ya mja wake ikiwa atahitaji kupata adhabu kama hio.

Mtu kukubali yakuwa yeye ndie mkosa.

Kumuomba Allaah kwa njia na vitu Anazo Zipenda mno, ambayo ni majina Yake na sifa Zake. Majina yake mawili ambayo yanachanganya maana ya majina na sifa Zake zote ni al-Hayy (aliye Hai) na al-Qayyoom (Mwenye kubakia milele)

Kuutafuta msaada wa Allaah peke Yake.

Kuhakikisha matarajio yako Kwake

Allaah.

Kumtegemea Yeye kikweli na kumuachia

Yeye mambo, kukubali kuwa paji lako la uso liko mkononi mwa Allaah na kuwa Yeye afanya atakavyo, yakuwa matako Yake yapita milele na kuwa yeye ni Muadilifu katika yote anayo Yakadiria.

Kuacha moyo wako kuranda randa katika bustani la Qur'an, kutafuta uliwazo ndani yake kutokana na kila msiba, kutafuta tiba kutoka huko kwa kila ugonjwa wa moyo, ili ilete utulivu kwa huzuni na shifaa kwa masumbufu na mahangaiko yake.

Kuomba msamaha (kwa kutubia)

Toba

Jihad

Swala

Kukubali kuwa hanauwezo wala nguvu, na kumuachia mambo kwa yule Ambaye wako mkononi Mwake.

Twamuomba Allaah atuweke

salama salimini kutokamana na

masumbufu na atupe afueni

kutokamana na mahangaiko na

wasiwasi na kubabaika, kwani Yeye

Ndiye Mwenye Kusikia bila

upungufu, Mweye Kujibu kila mara,

Naye Ndie aliye Hai, Wa Milele.